TANESCO
Tunayaangaza Maisha Yako

TOLEO NA.
06

Jarida la Mitandaoni

IJUMAA OKTOBA 23, 2020

## “Tunakuhudumia popote saa 24”



**SIMU:** +255 22 2 194 400/ +255 768 985 100

# Kituo cha Umeme Dege kumaliza kero za umeme Kigamboni, Ilala na Kurasini

Waziri wa Nishati Dkt.Medard Kalemani amesema kuwa mradi unaojengwa wa kituo cha kupooza umeme cha Dege-Kigamboni jijini Dar es salaam, utaimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Kigamboni, Kurasini na Ilala na hivyo kuondoa kero zote za umeme kwa wateja wa maeneo hayo.

Akizungumza katika eneo la ujenzi wa mradi huo alipokwenda kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi ,Oktoba 17, Waziri Kalemani amesema kuwa mradi huo umekamilika kwa asilimia 80 na kuitaka TANESCO kukamilisha mradi huo mapema zaidi.

**“Mradi huu unajengwa na TANESCO wenyewe,na wameniambia mradi huu utakamilika Disemba mwaka huu, lakini Mimi naagiza mradi huu ukamilike mwezi ujao yaani Novemba 2020” Dkt. Kalemani.**



# ZIARA KIGAMBONI



Aidha, alioogezea kuwa mradi huo utaimarisha upatikanaji wa umeme kwa maeneo ya Kigamboni, Ilala na Kurasini kwa kuwa kwa sasa wanasambaziwa umeme kutoka katika kituo kimoja Cha kupoza Umeme cha Kurasini lakini baada ya kukamilika kwa kituo hicho, maeneo ya Kigamboni hayatapata shida ya umeme tena.

“Natambua kuwa kuna maeneo ya Kigamboni hayana umeme lakin niwaambie tu kuwa tatizo la umeme linakwenda kuisha kwani mara baada ya kukamilika kwa mradi huu maeneo mengi ya Kigamboni yatapata Umeme” Dkt. Kalemani

Waziri Kalemani pia amesema sekta ya Nishati Nchini imeimarika kwakuwa kwa sasa Kuna vituo vya kupooza umeme 107, ambapo ndani ya miaka 5 vituo vikubwa 43 na vituo vidogo 7, vimejengwa ndani ya miaka mitano.

Ameongeza kwa kusema kuwa changamoto ya kuharibika kwa miundombinu wakati wa mvua inakwenda kuisha kwani matumizi ya Nguzo za zege yameaza kutumika.

“Mradi huu umetumia Nguzo za zege, kama mnavoziona hapo nje na Nguzo hizo zimeanza kutumika maeneo yenye majimaji, ili kuepuka hali ya kukosa umeme inayotokana na Nguzo kuoza kwasababu ya maji” Dkt. Kalemani





"TANESCO ni moja kati ya mashirika ya Umma ambayo yapo katika maboresho ya mifumo yake ya kiutendaji kazi ambayo yanalenga kuongeza ufanisi"
Mhe. Kimanta



# Bodi ya TANESCO yashiriki mafunzo ya uelekezi



Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imeshiriki na kupatiwa mafunzo ya uelekezi, lengo likiwa ni kujenga uwezo katika masuala mbalimbali ya usimamizi wa TANESCO.

Mafunzo hayo ya wiki moja yanafanyika kuanzia Oktoba 19, 2020, jijini Arusha.

Akifungua mafunzo hayo katika ukumbi wa AICC Jijini Arusha, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Idd Hassan Kimanta alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa Bodi ya TANESCO kutokana na baadhi ya wajumbe kuwa wageni katika Shirika pamoja na kukumbushana masuala mbalimbali ya uendeshaji wa TANESCO.

"TANESCO ni moja kati ya Mashirika ya Umma ambayo yapo katika maboresho ya mifumo yake ya kiutendaji kazi ambayo inalenga kuleta tija na kuongeza ufanisi" Mhe. Kimanta.

Mhe. Kimanta aliongeza kuwa mifumo ya ndani ya TANESCO inatakiwa kujengwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na kusisitiza kazi kubwa iliyopo kwa viongozi wa Bodi ni kuhakikisha wanasimamia sheria, kanuni na taratibu hizo.

Aidha, kutokana na TANESCO kuwa mdau muhimu katika maendeleo ya Tanzania kama ilivyo ainishwa katika Dira ya maendeleo ambayo inalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa juu, nishati ya umeme ikiwa ni nyenzo mojawapo inayotegemewa na hivyo kuhitajika usimamizi imara hasa katika miradi mikubwa na ya kimkakati kama wa Julius Nyerere na miradi mingine mingi inayolenga kuunganisha gridi ya Taifa katika Mikoa yote.

Mafunzo hayo, yatawawezesha Wakurugenzi hao wa bodi ya TANESCO kupata uelewa wa pamoja utakao ongeza ufanisi na tija katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku ndani ya TANESCO.











# Menejimenti TANESCO yaikubali kasi ya ujenzi Mradi wa Julius Nyerere

Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) imefanya ziara ya kukagua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji mradi wa kufua umeme wa Megawati 2115 kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) na kuonyesha kuridhishwa na kuikubali kasi ya utekelezaji wa mradi huo kulingana na mpango kazi uliopo.

Akiongea katika ziara hiyo, Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usambazaji na Huduma kwa Wateja, Mhandisi Raymond Seya, amesema kuwa ziara hiyo ina malengo mawili ambayo ni, kukagua hatua za utekelezaji wa mradi na kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi TANESCO.

Mhandisi Seya ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka, aliongeza kuwa, Menejimenti imeridhishwa na hatua za utekelezaji wa mradi tangu kuanza kwake ambapo ni zaidi ya mwaka na miezi mitano sasa.








“Mradi upo katika hatua nzuri, tumekagua maeneo mbalimbali mradi unapotekelezwa na tumejiridhisha, kazi zinaendelea na mradi utakamilika kama ilivyopangwa, Juni 2022” Mhandisi Seya.

Mhandisi Seya aliongeza kuwa, Menejimenti ya TANESCO inaishukuru Serikali kwa kumlipa Mkandarasi kwa wakati bila kumcheleweshea malipo, hali ambayo inachangia kasi ya utekelezaji wa mradi kwa Wakandarasi kuongezeka.

Kwa upande wa Mkuu wa Kazi za Ujenzi TECU, Mhandisi Lutengano Mwandambo alisema kazi za ujenzi wa mradi zinaendelea vizuri na kuongeza kuwa, ujenzi wa handaki la kuchepusha maji umefikia asilimia 95 na unatarajiwa kukamilika Oktoba 25 mwaka huu.



“Handaki hili la kuchepusha maji ni muhimu katika utekelezaji wa mradi huu, kwani ndio litawezesha ujenzi wa tuta la kuzuia maji kujengwa, tunatarajia hadi kufikia Oktoba 25 mwezi huu kazi ya kumimina zege kwenye handaki itakuwa imekamilika” Mhandisi Mwandambo.

Aidha, Mkandarasi amechukua hatua muhimu badala ya kusubiri maji kuchepushwa kwenye handaki, tayari ameanza ujenzi wa tuta sehemu ya pembeni mwa mto tangu Oktoba 13, 2020.


Ziara ya Menejimenti inafuatia ziara ya Bodi ya Wakurugenzi TANESCO kwenye mradi wa Julius Nyerere Oktoba 04, 2020, ambapo Bodi ilitoa maelekezo ya kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.







# TANESCO **Rukwa yafungua** ONE STOP SHOP



Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Rukwa kupitia Meneja Mwandamizi Kanda ya Mangaribi, Mhadisi Sana Idindili limezindua Ofisi mpya ya huduma za pamoja (one stop shop) kwa lengo la kuimarisha huduma kwa wateja Mkoani humo.

Katika uzinduzi huo Mhandisi Idindili ametoa pongezi kwa uongozi wa Mkoa wa Rukwa kwa kuweza kusimamia ujenzi wa ofisi hiyo muhimu kwa huduma kwa wateja.

Aliongezea kuwa TANESO nchi nzima imejipanga kuwapatia wateja umeme wa uhakika na kuboresha huduma kupitia kufungua ofisi za one stop shop ili kupunguza usumbufu kwa wateja wake nchi nzima.



> **“Nategemea ofisi hii ya one stop shop itaimarisha huduma kwa wateja Mkoani Rukwa, Wateja wetu wataweza kuhudumiwa kwa haraka na wakati bila kupoteza muda, kwani huduma zote zitakuwa zinapatikana kwenye jengo hili” Mhandisi Idindili.**



Naye Meneja wa Mkoa wa Rukwa Mhadisi Yusuf Ismail aliwataka wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kutumia ofisi ya onestop shop kupata huduma mbalimbali za TANESCO kupitia eneo moja kwani itasaidia punguza harama na muda ambao wanaweza kutumia katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

# Miongozo ya Mazingira inazingatiwa JNHPP




## Njia ya kuchepusha maji, utekelezaji wake umefikia asilimia **95**, kukamilika Oktoba **25, 2020**

Utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme wa Megawati 2115 kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) umeambatana na tathmini ya athari za mazingira (Environmental Impact Assessment) inayozingatia ikolojia ya eneo la mradi na kuhakikisha shughuli za utekelezaji wa mradi haziathiri mazingira kwa namna yoyote ile.

Akizungumzia ambavyo wanalikabili suala la mazingira, Meneja Usalama na Mazingira wa mradi wa JNHPP, Mhandisi Majige Mabula alisema utekelezaji wa mradi unaambatana na utunzaji wa mazingira kuzingatia na kulingana na Tathmini ya Athari za kimazingi (EIAA) pamoja na sheria zote za mazingira za kitaifa na kimataifa.

**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
Dkt. Tito E. Mwinuka
Mkurugenzi Mtendaji TANESCO

**Mhariri Mkuu:**
Johary Kachwamba
Meneja Uhusiano

**Wachangiaji:**
Grace Kisyombe
Yasini Silayo
Salama Kasamalu
Samia Chande

**Msanifu wa kurasa:**
Henry Kilasila

Mhandisi mabula aliongeza kuwa, kazi zinazofanyika eneo la mradi haziharibu mazingira na zimezingatia kanuni zote za utunzaji mazingira kutokana na eneo hilo kuwepo pia kwa wanyama ambao uwepo wao unategemea mazingira hayo.

**"Tunajitahidi kukabiliana na visababishi vya uharibifu wa mazingira, mfano kelele tunapima mara kwa mara ili tusisababishe kelele kubwa ambayo itapelekea wanyama kukimbia kwenye maeneo haya" Mhandisi Mabula.**

Aidha, kulingana na tathmini ambazo zimefanyika zinaonesha eneo ambalo mradi unatekelezwa lina mazingira salama, kiasi kwamba wanyama bado wanaendelea kuwepo kwenye maeneo hayo pamoja na kazi za mradi kuendelea kwa kwa kipindi cha takriban mwaka wa pili sasa.

Eneo lingine linaloangaliwa katika uharibifu wa mazingira ni maji, kutokana na maji ya mto Rufiji kutumika na wananchi wa eneo la chini ya bonde la mto rufiji. Usalama wa maji kwa kupimwa mara kwa mara.

Alieleza kuwa takwimu zinazotokana na upimaji zinaonesha, shughuli za utekelezaji wa mradi haziharibu maji hayo.

Kutokana na mradi kutekelezwa eneo la mbugani suala la usalama pia limezingatiwa ili wanyama wakali wasilete madhara kwa Wafanyakazi wa mradi wakati wote wa utekelezaji mradi.

**"Tunaangalia maeneo mengi ikiwemo vumbi na kingo za barabara, tunahakikisha zinamuwezesha mnyama kuvuka kutoka kingo moja kwenda nyingine" Mhandisi Mabula.**

Kwa upande wake, Afisa Usalama JNHPP, Bwana Fidelis Almasi alisema, askari wa wanyamapori wa TANAPA wamekuwa wakilinda eneo ambalo mradi unatekelezwa dhidi ya wanyama wakali.

Aidha, Wafanyakazi wote na wageni wanaoingia katika eneo la mradi wanapewa mafunzo ya awali ya usalama kazini ikiwemo na kupewa vifaa vya usalama mahala pa kazi.

Mradi wa Julius Nyerere mbali ya kuipatia Nchi umeme wa uhakika, utaongeza idadi ya watalii wa nje na wa ndani.

Akizungumzia jinsi ambavyo shughuli za utalii zitaongezeka, Mhandisi Mkazi kwenye mradi wa Julius Nyerere, Mhandisi Mushubila Kamuhabwa, anasema baada ya tuta kutengezwa maji yatazuiwa na hivyo kutengenezwa ziwa ambalo limepewa jina la Ziwa la Nyerere.

Alisema ziwa hilo la Nyerere litakuwa na kilometa za mraba 1,200 na kuongeza litakuwa la tano kwa ukubwa Tanzania.

**"Ziwa hili litakuwa na maji ambayo sio ya chumvi, litakuwa na visiwa mbalimbali idadi yake inafika kumi na nane, kwa hali hiyo litachangia katika shughuli za utaliii" Mhandisi Kamuhabwa.**

TANESCO Tunayaangaza Maisha Yako

Plot No. 114, Block G, Dar es Salaam Road, P.O.Box 453 Dodoma, Email: info@tanesco.co.tz

**SIMU:** +255 22 2 194 400/ +255 768 985 100

Whatsup group zipo nchi nzima | tanescoyetultd | tanescoyetu | tanesco_official_page | tanesco yetu